

**Mkutano na Idara ya Usafiri wa Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam
10 Machi 2008**

Mahudhurio

Mama Mlamba	Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam
Elaine Baker	UWABA
Filbert Mbecha	UWABA
Jumanne Idd	UWABA
Juma Ally Salehe Jongo	UWABA
Paulo Atibu	UWABA

Mrs Mlamba alieleza kuhusu mradi wa DART na aliwaambia UWABA kwamba unatoa kipau mbele kwa njia za baisikeli na “mainstreaming” baisikeli kama chombo cha usafiri. Njia za baisikeli zipo ndani ya mipango na michoro ya Barabara ya Morogoro. Alisema kuweka njia za baisikeli kwenye barabara moja moja haitoshi – lazima kuunganisha njia za baisikeli kwa jiji nzima. Alisema kwamba Road Safety Audit ilifanyikwa kwenye mipango. Alitonyesha video kuhusu mradi wa DART. Video inasema kwamba kuna mpango kwa njia za baisikeli kwa 120 km.

Mrs Mlamba alisema tushirikiana na AALOCOM ambalo ni shirika la wataalam wa usafiri wanaopendelea uendeshaji wa baisikeli. UWABA tayari tumeshirikiana na AALOCOM kwa kutengeneza msafara wa baisikeli.

Mrs Mlamba alipendekeza UWABA tufanye kampeni kufuta kodi kwenye baisikeli kwa kushirikiana na mashirika mengine. Alisema kwamba Kenya hakuna kodi kwenye baisikeli na tujaribu kupata sera hii hapa pia. Wanachama wa UWABA walisema wataanzisha kampeni hii.

Elaine alipendekeza njia za baisikeli zifai kwa baisikeli za walemavu na maguta (baisikeli za gurudumu tatu). Mama Mlamba alisema kwamba maguta yanaleta shida kwa usafiri mwingine na yeye hapendekezi matumizi ya maguta. Elaine alisema kwamba maguta ni aina ya baisikeli na wanachama wengi wetu wanapata maisha yao kwa kusafirisha bidhaa kwa guta. Elaine alisema kupiga marufukuu maguta ingehamasisha pick-up ambazo zinachukua nafasi kubwa zaidi barabarani, zina gharama kubwa zaidi, zinatumia mafuta na pia sera hii ingeongeza umasikini wa wadereva wa maguta. Mama Mlamba alisema kwamba anafikiri wapanda baisikeli wengine kama walemavu wanaogopa kuwa pamoja na maguta. Paulo alisema kwamba hili ni swala la elimu na kuhamasisha wapanda guta kuheshima wengine wanaotumia barabara, na kwamba UWABA tumeshaanzisha kazi hii kwa sababu wapanda guta wa UWABA walihudhuria semina ya usalama barabarani Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

Kuhusu swala la baisikeli za walemavu Mama Mlamba alisema ataangalia michoro kuhakikisha upana wa nguozo ili walemavu wanaweza kupita.

Tulizungumza kuhusu uvazi unaofaa kwa ofisi kwa sababu wanachama wengine wa UWABA walifika kwenye mkutano na fulana na suruali fupi.. Elaine alieleza kwamba ni kita cha kawaida kuendesha baisikeli na fulana na suruali fupi, na hajafahamu wapi kuna sehemu kwenye jengo hili pa kuoga na kubadalisha nguo. UWABA walikubali kuja kwenye mikutano mengine na shati na suruali ndefu.

Elaine na Paulo walisema kwamba magari sasa wanatumia service road kupaki gari na kupita foleni, na kwamba wanaweza kuendelea kufanya hivi kwenye njia za baisikeli. Paulo pia alisema kuna waendesha magari wengi hawatoi heshima kwa wapanda baisikeli na alisema kwamba hii ni sababu kubwa kwa nini wanawake wengi hawapandi baisikeli. Mama Mlamba alikubali na alisema hapendi jinsi ambavyo waendesha magari wanapiga honi na hawatoi heshima kwa wapanda baisikeli. Mama Mlamba alisema kwamba atahakakisha kwamba magari hawawezi kuingia njia za baisikeli za Morogoro Road zitakapojengwa.

Tulizungumza kuhusu mazingira ya wapanda baisikeli Ulaya. Elaine alisema kwamba majiji mengine Ulaya wana mazingira mazuri kwa wapanda baisikeli lakini majiji mengi yana mazingira mabaya sana na haifai kuyafuata. Mama Mlamba alisema kwa sababu jiji la Dar es Salaam bado linaendelea basi kuna nafasi kubwa kujenga mazingira mazuri kwa wapanda baisikeli kuliko majiji ambayo yameshajengwa kwa kuangalia mahitaji ya magari tu. Alisema kwamba dunia nzima watu wengi wanahamasisha wapanda baisikeli, hasa kwa sababu ya matatizo ya mabadaliko ya majira.

Mama Mlamba alisema ni muhimu kwamba baada ya serekali kuweka njia za baisiekli zitumikwe sana, ili serekali inapata thamani ya hela zake. Wanachama wa UWABA walisema wana uhakika kwamba njia za baisikeli zitatumikwa vizuri na kwamba tutaendelea kuhamasisha baisikeli kama chombo cha usafiri kwenye Msafara ya Baisikeli. Elaine alionyesha picha ya Mhe Azzan Zungu Mbunge wa Ilala akiendesha baisikeli kwenda bungeni na alisema viongonzi kama huyu wanaweza kutoa mfano mzuri kwa wananchi. Alisema itakuwa nzuri kama viongonzi na wafanyakazi wa ofisi wapande baisikeli ili kuhamasisha wengine.

Elaine alionyesha Mama Mlamba kurasa za tovuti ya UWABA na picha za Msafara wa Baisikeli.

Mama Mlamba alisema ataendelea kualika UWABA kwenye mazungumzo ya washika dau na mazungumzo kuhusu Mpango wa Usafiri wa Dar es Salaam. Alisema kwamba ni muhimu wapanda baisikeli wawepo ili watu waone masuala ya usafiri kwa kutumia macho ya wapanda baisikeli.

UWABA tulishukuru sana Mama Mlamba kwa ajili ya mkutano.